**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**WIZARA YA KILIMO**

**BODI YA KOROSHO TANZANIA**

# TAARIFA KWA UMMA

Bodi ya Korosho Tanzania (CBT) inapenda kuujulisha Umma kuwa kuanzia tarehe ya tangazo hili 19 Februari 2025, mikataba yoyote kuhusu biashara ya Korosho, ikiwa ni pamoja na, ununuzi wa korosho ghafi na karanga (kernels) pamoja na bidhaa zingine zitokanazo na korosho, usindikaji, usafirishaji, umiliki na uendeshaji wa ghala, itatakiwa kupitiwa na kusajiliwa CBT.

Hivyo Wadau wote wa Tasnia ya Korosho wanakumbushwa kuwa Vibali na leseni ya kununua, kusafirisha, kuuza, kusindika, kumiliki au kuendesha ghala na hata kupeleka korosho nje ya nchi kwa misingi ya kufanya biashara vinatolewa na Bodi ya Korosho Tanzania kwani Mikataba tajwa haitakuwa halali hadi pale itakapowasilishwa CBT kwa mapitio na kuthibitishwa.

Aidha, CBT inawakumbusha wadau wote katika mnyororo wa thamani wa zao la korosho kuzingatia sheria, kanuni na miongozo inayotolewa kwa maendeleo ya Tasnia ya Korosho na Taifa kwa ujumla na kuwa haitasita kuchukua hatua stahiki za kisheria kwa mtu, kikundi, taasisi, au kampuni itakayoshindwa kuzingatia maelekezo haya.

Bodi ya Korosho Tanzania (CBT) ni Taasisi ya Serikali chini ya Wizara ya Kilimo iliyokasimiwa jukumu la kusimamia maendeleo ya Tasnia ya Korosho nchini na imeanzishwa kwa Sheria ya Tasnia ya Korosho No.18 ya mwaka 2009 na Kanuni zake za mwaka 2010. Na inatekeleza majukumu yake kama ilivyo ainishwa chini ya kifungu cha 5(2) (e) na kifungu cha 12, na 15 cha Sheria No.18 ya Mwaka 2009 na Kanuni zake za Mwaka 2010.

Imetolewa na:
**MKURUGENZI MKUU**
**BODI YA KOROSHO TANZANIA**
**19 Februari, 2025**